



**Kongamano la kwanza kuhusu ushiriki  
wa vijana katika michakato ya amani**

**RIPOTI YA TUKIO LA KANDO**

---

---

# **Ushiriki wa Vijana katika Ushirikiano wa Kimazingira na Michakato ya Amani**

***7 Machi 2019, Helsinki, Ufini***

---

---

**Yaliyomo**

Muhtasari Mahsusi

1. Utangulizi	4
2. Mawasilisho na Mjadala	5
3. Mjadala wa Kikundi Kidogo cha World Café	11
4. Mjadala wa jopo	14
5. Hitimisho	15

Shukrani

Waandaaji

Ratiba



**Kongamano la kwanza kuhusu ushiriki wa vijana katika michakato ya amani**

**RIPOTI YA TUKIO LA KANDO:**

## **Ushiriki wa Vijana katika Ushirikiano wa Kimazingira na Michakato ya Amani**

**7 Machi 2019, Helsinki, Ufini**

**Mratibu wa Tukio**

Antti Erkkilä

**Waandishi Viongozi**

Antti Erkkilä

Juha M. Kotilainen

Emma Luoma

**Waratibu wa Meza ya World Café**

Denis Dobrynin

Violeta Gutiérrez

Daniela Tináková

**Mwandishi Mkuu**

Irmeli Mustalahti

Profesa wa Usimamizi wa Maliasili

Chuo Kikuu cha Ufini Mashariki

[irmeli.mustalahti\[at\]uef.fi](mailto:irmeli.mustalahti[at]uef.fi)**Kikundi cha utafiti:**[www.uef.fi/en/web/responsive-natural-resources-governance](http://www.uef.fi/en/web/responsive-natural-resources-governance)**Picha ya ukurasa wa mbele:** Antti Erkkilä, 2018**Picha ya ukurasa wa nyuma:** Shutterstock

## Muhtasari Mahsusi

Tukio la wazi la Kando kuhusu Ushiriki wa Vijana katika Ushirikiano wa Kimazingira na Michakato ya Amani lilifanyika mnamo tarehe 7 Machi 2019 Jijini Helsinki, Ufini. Washiriki vijana walitoka nchi za Kolombia, Ufini, Indonesia, Kenya, Liberia, Meksiko, Myanma, Ufilipino, Urusi, Slovakia, Sudani Kusini, na Sri Lanka. Tukio hili liliandaliwa na miradi ya utafiti ya MAKUTANO, ALL-YOUTH, na CORE, ambayo inafadhiliwa na Akademia ya Ufini, Baraza la Utafiti wa Kimkakati (SRC), pamoja na ALLIANSSI, ambalo ni Shirika la Vijana wa Kifini. Ushiriki wa vijana waleta-amani wa kimataifa uliwezesha na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufini, Ofisi ya Mjumbe wa Vijana wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (OSGEY), na Umoja wa Mtandao wa Vijana-waleta Amani (UNOY).

Mjadala wa wazi ulikuwa moja ya matukio ya kando katika Kongamano la Kwanza kuhusu Ushiriki wa Vijana katika Michakato ya Amani lililoandaliwa Jijini Helsinki tarehe 5-6 Machi 2019 na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufini na Umoja wa Mataifa, pamoja na wawakilishi wa jumuiya za kiraia. Wenyeji wa tukio hili walikuwa Serikali za Katari na Kolombia.

Kongamano la Kimataifa, Kuendeleza Maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa 2250 (2015) na 2419 (2018) kuhusu Vijana, Amani, na Usalama lilichunguza wajibu ambao vijana wanaweza kuwa nao na ambao wanao sasa hivi katika michakato ya amani. Maazimio Na. 2250 na 2419 yanasisitiza wajibu muhimu wa vijana katika jamii zao na yanazitaka nchi wanachama kufikiria njia za kuongeza ujumuishaji wa vijana.

Wakati wa Tukio la Kando, washiriki vijana waliwasilisha uzoefu, ukweli, matarajio yao, pamoja na mafunzo waliyojifunza ulimwenguni kuhusu masuala yanayohusiana na ushirikiano wa kimazingira na michakato ya amani. Mawasilisho yalikushusu shughuli za mabadiliko ya tabianchi na ukweli nchini Ufini na Sri Lanka; masuluhisho ya kivumbuzi ya amani dhidi ya migogoro nchini Kolombia na Sudani Kusini; masuala ya jinsia na jamii finyu katika utunzaji wa amani nchini Lebanoni na Kosovo; Jamii ya Wasámi na maslahi kinzani dhidi ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya Kaskazini mwa Ufini; pamoja na mafunzo yaliyotokana na kozi za Nchi za Kinodi kuhusu ushirikiano wa kimazingira na usuluhishi wa migogoro. Tukio lilikushusu pia mijadala ya vikundi juu ya maswali matatu mahususi yaliyohusu ushirikiano wa kimazingira na michakato ya amani. Masuala yaliyoibuka yalijadiliwa katika mijadala ya majopo. Ilihitimishwa kwamba umuhimu wa kusikiliza kwa makini hauwezi kupuuzwa. Masuala na majanga ya kimazingira yanaweza kuwa vyanzo vya migogoro ya kisiasa ya kitaifa na kimataifa. Hivyo, masuala ya kimazingira yatahitaji mkazo mkubwa zaidi katika michakato mingi ya amani.

Ripoti hii inawasilisha muhtasari wa ajenda, mawasilisho, na hoja muhimu za mijadala. Kwa taarifa zaidi au maswali, tafadhali wasiliana na [antti.erkkila@juef.fi](mailto:antti.erkkila@juef.fi) na [irmeli.mustalahti@juef.fi](mailto:irmeli.mustalahti@juef.fi).

## 1. Utangulizi

Tukio la wazi kuhusu Ushiriki wa Vijana katika Ushirikiano wa Kimazingira na Michakato ya Amani liliandaliwa tarehe 7 Machi 2019 katika ukumbi wa Think Corner wa Chuo Kikuu cha Helsinki, nchini Ufini.

Tukio hili liliandaliwa na miradi ya utafiti ya MAKUTANO, ALL-YOUTH, na CORE, ambayo yote inafadhiliwa na Akademia ya Ufini na Baraza la Tafiti za Kimkakati (Strategic Research Council - SRC) pamoja na ALLIANSSI, Shirika la Vijana la Ufini (the Finnish Youth Co-Operation).

Mjadala wa wazi ulikuwa moja ya matukio ya kando katika Kongamano la Kwanza kuhusu Ushiriki wa Vijana katika Michakato ya Amani lililoandaliwa katika “House of the Estates” Jijini Helsinki tarehe 5-6 Machi 2019 na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufini na Umoja wa Mataifa pamoja na wawakilishi wa jumuiya za kiraia (bofya [HAPA](#) ili kupata ripoti). Wenyeji wa Kongamano walikuwa Serikali za Katari na Kolombia. Kongamano la Kimataifa, Kuendeleza Maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa 2250 (2015) na 2419 (2018) kuhusu Vijana, Amani, na Usalama lilichunguza wajibu ambao vijana wanaweza kuwa nao na ambao wanao sasa hivi katika michakato ya amani.

Maazimio Na. 2250 na 2419 yanasisitiza wajibu muhimu wa vijana katika jamii zao na yanazitaka nchi wanachama kufikiria njia za kuongeza ujumuishaji wa vijana (bofya [HAPA](#) kupata Waraka wa Sera ya Dunia kuhusu Michakato ya Amani Inayowajumuisha Vijana).

Waandaaji wa Tukio la Kando kuhusu Ushiriki wa Vijana katika Ushirikiano wa Kimazingira na Michakato ya Amani wanaamini kuwa uwakilishi jumuishaji wa vijana unapaswa pia kutambuliwa katika usuluhishi wa migogoro ya kimazingira. Kiukweli, stadi za ushirikiano wa kimazingira na usuluhishi wa migogoro ya kimazingira zinapaswa kuchukuliwa kama elimu ya uraia.

Katika kuandaa Tukio la Kando la Kongamano la Kimataifa, tulitaka kuonesha kuwa masuala na majanga ya kimazingira yanaweza kuwa vyanzo vya migogoro ya kisiasa, kitaifa, au kimataifa. Hivyo, masuala ya kimazingira yanaweza kuhitaji mkazo mkubwa zaidi katika michakato mingi ya

amani. Aidha, tulikuwa na shauku ya kuandaa tukio la kando ambalo vijana wajenzi wa amani wa kimataifa watapata fursa ya kuchangamana zaidi na vijana wenyeji, na kubadilishana ujuzi na uzoefu wao.

Tukio hili la Kando kuhusu Ushiriki wa Vijana katika Ushirikiano wa Kimazingira na Michakato ya Amani lilifunguliwa na **Reetta Toivanen**, Kiongozi wa Shirika la Utafiti la ALL-YOUTH (STN) na Profesa wa Sayansi Endelevu wa Chuo Kikuu cha Helsinki. ALL-YOUTH – Vijana Wote Wanataka Kutawala Dunia Yao – ni mradi wa utafiti wa taaluma mchanganyiko unaochunguza uwezo na vikwazo dhidi ya vijana katika kushirikiana na jamii. Shirika la Utafiti la ALL-YOUTH linajumuisha Chuo Kikuu cha Helsinki, Chuo Kikuu cha Tampere, na Chuo Kikuu cha Ufini Mashariki.

Baada ya Reetta kutoa hotuba ya ufunguzi, vijana wa kimataifa na wenyeji waliwasilisha mawasilisho yao mafupi kuhusu kuleta amani na ushirikiano wa kimazingira kwa mujibu wa uzoefu wao. Mawasilisho na mjadala wa wazi uliofuata uliongozwa na **Heta Heiskanen** kutoka Shirika la Utafiti la ALL-YOUTH. Baada ya mapumziko mafupi, mjadala zaidi na mahususi wa Kikundi Kidogo cha World Café ulifanyika kuhusu masuala matatu. Majadiliano ya vikundi na mjadala wa jopo uliofuata uliongozwa na **Irmeli Mustalahti**, ambaye ni Mratibu wa Mawasiliano wa Mradi wa Kimataifa wa Shirika la Utafiti la ALL-YOUTH na Profesa wa Usimamizi wa Maliasili katika Chuo Kikuu cha Ufini Mashariki.

Washiriki wa Tukio la Kando walitoka Kolombia, Ufini, Indonesia, Kenya, Liberia, Meksiko, Myanmar, Ufilipino, Urusi, Slovakia, Sudani Kusini, na Sri Lanka. Ushiriki wa vijana wajenzi wa amani wa kimataifa uliratibiwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufini, Ofisi ya Mjumbe wa Vijana wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (OSGEY), na Umoja wa Mtandao wa Vijana Vijana-waleta Amani (UNOY).

Tukio la Kando liliratibiwa na **Antti Erkkilä** wa mradi wa utafiti wa MAKUTANO. Huu ni mradi uliotokana na mahitaji ya Watanzania ya ushirikiano na usuluhishi wa migogoro ya kimazingira. Mradi wa MAKUTANO unafadhiliwa



na Programu ya Akademia ya Maendeleo iliyobuniwa kwa pamoja kati ya Akademia ya Ufini na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufini.

## 2. Mawasilisho na Mjadala

Baada ya hotuba ya ufunguzi, washiriki vijana walipanda jukwaani na kuwasilisha uzoefu, ukweli, matarajio yao, pamoja na mafunzo waliyojifunza ulimwenguni kuhusu masuala yanayohusiana na ushirikiano wa kimazingira na michakato ya amani.

### **Shughuli za Vijana wa Kifini kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi**

Kipindi cha mawasilisho kilianza na **Joel Linnainmäki**, mtaalamu wa ushawishi wa kimataifa katika Shirika la Vijana la Kifini la ALLIANSSI.

Joel aliwaelezea washiriki kazi zinazofanywa na vijana wa Kifini katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Alieleza kuwa, kwanza kuna wawakilishi wa vijana wanaofanya kazi “chumbani”; mathalani, katika Ajenda ya Kifini 2030 ya Kundi la Vijana iliyowekwa wakati wa majira ya kuchipua majani ya mwaka 2017

chini ya Tume ya Taifa ya Maendeleo Endelevu (FNCSD) iliyoongozwa na Waziri Mkuu wa Ufini. Aidha, Mwakilishi wa Vijana wa Kifini huhudhuria mikutano ya Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Vijana pia hutekeleza majukumu yao “nje ya chumba”, wakiandaa aina mbalimbali za matukio yanayowapa sauti kuhusu masuala ya tabianchi na kujaribu kuvishawishi vyama vya siasa. Kwa ujumla, vijana wanawajibika sana kuhusu masuala ya tabianchi, na kwa namna mbalimbali wamekuwa wakiongoza majadiliano nchini Ufini.

Ingawa yote haya ni mambo mema, Joel aliuliza swali muhimu kuhusu haki ya yote haya: Je, tunaweza kwa hakika kuwaachia vijana pekee uanaharakati, kwa kuwaacha wabebe wajibu na mzigo wa kazi ya ushawishi kwa watunga sera na watumishi wa umma? Jibu lake lilisadifu majibu ya wanamjadala:

*“Ninadhani hatutakuwa tumetenda haki kwa vijana kwa sababu hili si jukumu lao wao pekee yao, bali ni jukumu la kila mmoja katika jamii.”*

Suala lingine lililobuliwa na Joel ni kuwa mabadiliko ya tabianchi litakuwa suala la uzoefu

wa kizazi kwa vijana, kama ilivyo kwa matukio mengine makubwa yaliyotafsiri uzoefu wa vijana katika miaka ya 1980 au 1990. Kuna uwezekano mkubwa kwa vijana kuwa watakumbuka ushiriki wao katika harakati za kijamii – kuwashawishi watu kutenda zaidi – katika muda wa miaka 20 au 30 ijayo.

Mwisho, Joel alitukumbusha kwamba ingawa uanaharakati ni muhimu, tunahitaji michakato rasmi pia. Vijana wanapopiga kura, humaanisha vyama vya siasa vinapaswa kuwajali pia. Hivyo, vijana wanaweza kuathiri mijadala muhimu badala ya kuwaachia watu wengine watafsiri maslahi yao.

### **Ukweli kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi Nchini Sri Lanka**

Baada ya vijana wa Kifini, tulisikia ukweli kuhusu mabadiliko ya tabianchi nchini Sri Lanka, uliowasilishwa na **Suchith Abeyewickreme**, mkufunzi wa kimataifa wa masuala ya kuleta amani, elimu ya maadili, na majadiliano ya kidini. Mara nyingi, masuala ya tabianchi yanapoibuka na uanaharakati unapogonga vichwa kwenye vyombo vya habari, kunakuwa na umakini katika matendo ya Ukanda wa Kaskazini mwa dunia. Hata hivyo, Suchith alibainisha kwamba kwa hakika ni Ukanda wa Kusini ndio ulio katika hatari zaidi na unaoathirika zaidi kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Nchini kwake, Sri Lanka, inakadiriwa, katika baadhi ya vipimo, inashika nafasi ya pili ulimwenguni kwa kuwa katika hatari kutokana na mabadiliko ya tabianchi; mafuriko pamoja na ukame uliokithiri vimekuwa na athari kubwa kwa uchumi wa nchi ambayo inategemea zaidi mzunguko wa mazao. Maisha ya wakulima yameendelea kuwa magumu na yasiyotabirika. Mbaya zaidi, hofu hii imesababisha hata watu kujiua kutokana na mazao kuharibika mashambani na mzigo wa madeni. Vilevile, wakazi wa mijini walio katika mazingira hatarishi ndio wanaoathirika zaidi. Mathalani, watu maskini kabisa, wanaoishi katika makazi holela kandokando ya mito hukabiliwa na hatari kubwa zaidi ya kukumbwa na mafuriko.

Hoja kuu ya pili iliyowasilishwa na Suchith ilisisitiza uhusiano kati ya mabadiliko ya tabianchi na migogoro, kuleta amani, na ushirikiano. Ukichunguza maeneo mengi yenye migogoro kama vile Siria na Yemeni, si migogoro

inayohusiana na masuala ya kisiasa pekee; bali inahusiana sana na rasilimali na mazingira hata kama inaoneshwa vinginevyo. Haijatokea kinasibu kwamba mabadiliko ya tabianchi yameathiri kwa kiasi kikubwa maeneo haya.

Ni muhimu tujenge ushikiano kati ya Ukanda wa Kaskazini na Ukanda wa Kusini katika uanaharakati wa kitabianchi ili sauti za kusini na maeneo yaliyo hatarini zaidi zisipotee katika mchakato huu. Wakati uanaharakati wa mabadiliko ya tabianchi katika Ukanda wa Kaskazini unaweza kushikilia juujuu bango hili, katika baadhi ya miktadha ya Ukanda wa Kusini wa dunia, uanaharakati wao unaweza kuwa katika mfumo wa 'Amani', 'Haki za Binadamu', na 'Umaskini'. Uanaharakati wao unaweza usishikilie kwa namna ileile bango la 'Mabadiliko ya Tabianchi'. Hii ina maana kuwa Uanaharakati wa Dunia wa Mabadiliko ya Tabianchi unahitaji kushikamana na uanaharakati mwingine, badala ya kuwa wa utengano, ambao unawakilisha sauti za tabaka la wanaojiweza pekee na kuwatenga watu walio katika mazingira hatarishi. Aidha, wakati mwingine sayansi ya kiwango cha juu ya mabadiliko ya tabianchi haiwashirikishi katika majadiliano watu walio katika mazingira hatarishi. Suchith alihitimisha kwa kusema:

*“Tunapaswa kuhakikisha kuwa tunaita mitazamo yote ya Ukanda wa Kaskazini na Ukanda wa Kusini kuhusu masuala ya tabianchi, na tunaendesha harakati za pamoja katika sekta zote tunazofanyia kazi.”*

### **Jinsia na Masuala ya Jamii za Wachache katika Utunzaji wa Amani Nchini Lebanoni na Kosovo**

Wasilisho la **Kethlin Piirma** lilihusu uzoefu wake kutoka Lebanoni, Kosovo, na Bosnia & Herzegovina, ambako amefanya kazi katika mashirika ya kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa, NATO na OSCE.

Alianza kwa kueleza kuwa pande zote katika mgogoro zinapaswa kuwa sehemu ya suluhu. Ndiyo maana mashauriano ni suala la msingi katika usuluhishi wa migogoro. Katika usimamizi jumuisi wa majanga, jeshi, polisi, na raia wote hushiriki na hudhamiria kuwalinda raia na kulinda mamlaka ya mpango wa ulinzi. Kufanya kazi kwa pamoja kunaonekana kuwa njia madhubuti

zaidi ya kupata suluhu ya migogoro na amani endelevu.

Wanaume na wanawake pamoja na jamii mbalimbali, marika, au jamii za wachache mara nyingi huwekwa katika nafasi tofauti katika mazingira ya migogoro. Kwa kutumia mifano halisi, Kethlin anabainisha kuwa makundi tofauti yana mahitaji, mitazamo, na matatizo tofauti. Ukweli huu unafanya kuleta amani kuwa suala mtambuka. Masuluhisho hayawezi kuwa sawa kwa migogoro yote, na kwa mara nyingine tena, ndiyo maana majadiliano ni msingi wa mafanikio.

Kwa kuzingatia uzoefu wa Kethlin, vijana, wawe wa jamii tofauti kama vile Wasebia au Waalbania nchini Kosovo; au dini tofauti kama vile Wakristu au Waislamu nchini Lebanoni, wote wana shauku ya kulinda amani na kutumia kwa pamoja mazingira yaliyopo. Alihitimisha wasilisho lake kwa kusisitiza kuwa:

*“Iwapo wanawake, jamii za wachache, na vijana hawatashirikishwa kikamilifu kama wajenzi wa amani, hatutapata amani ya kudumu.”*

### **Kampeni ya Nadafa Le Beledna Nchini Sudani Kusini**

**Wani Michael**, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Okay Africa (OAF) na mwanzilishi wa Kampeni ya Nadafa Le Beledna, alitonesha filamu fupi (kuangalia video bofya [HAPA](#)) kuhusu kampeni nchini Sudani Kusini, ambako kuna ongezeko la haja ya vijana kushiriki katika juhudi za pamoja za kusafisha mitaa ya jiji.

Katika mkanda wa video, tuliweza kuona kwamba kampeni haikuhusu tu kuweka mazingira safi bali pia kuwaleta pamoja vijana nchini Sudani Kusini ili wajisikie kuwa wana fursa ya kuleta utofauti.

Video inaonesha kikundi cha vijana kikizunguka mitaani kikiwa na mifuko ya taka, fagio, na malori kikizoa taka na uchafu. Ingawa mtu anaweza kuona kuwa kazi ni ngumu, na joto kali ni changamoto, jambo linalojibainisha pia ni furaha na burudani ambayo vijana wanayo. Tunaona muziki ukipigwa na vijana wanacheza kwa furaha.

Wakati akiwasilisha video yake, Wani Michael alisisitiza kwamba dhima ya kampeni ni kuwapa vijana fursa ya kuwa watu muhimu kwa jamii yao. Katika nchi na jamii ambazo mamlaka yamegawanywa bila usawa na serikali inaweza kuwa ya kifisadi, ni muhimu kutafuta njia salama na zisizo na vizingiti ili uanaharakati uweze kufanyika. Kusafisha mitaa ni njia mojawapo ya kuleta utofauti na kushiriki katika mjadala wa wazi kuhusu mazingira.

### **Jamii ya Sámi na maslahi kinzani ya matumizi ya ardhi Kaskazini mwa Ufini**

Wasilisho lililofuata lilitolewa na **Petra Laiti**, ambaye ni mwenyekiti wa Shirika la Vijana wa Kisámi Nchini Ufini.

Yeye alijadili historia na wajibu wa jamii ya Sámi nchini Ufini na aliibua maswali muhimu kuhusu jinsi ya kutatua maslahi kinzani na kujenga hali ya kuaminiana kati ya jamii za wenyeji na dola.

Kwa kuwa jamii ya Wasámi inaweza isifahamike kwetu sote, Petra alianza kwa kueleza kuhusu hali na usuli wa mgogoro katika eneo la Sámi. Alieleza kuwa Wasámi ni jamii ya wenyeji wanaoishi katika maeneo ya kaskazini mwa Ufini, Swedeni, Norwei, na Urusi. Jamii ya Wasámi ina jumla ya watu takribani 100,000; na eneo la Wasámi lina ardhi ya ukubwa wa kilometa za mraba 400,000. Shughuli yao kuu ya kienyeji ni ufugaji wa kulungu na uvuvi. Ufugaji wa kulungu, hususani, unahitaji maeneo makubwa ya ardhi ambamo kulungu watazaga. Kama Petra alivyoelezea, katika haki 46 zilizo rodheshwa katika Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Jamii za Wenyeji, tisa ni mahususi kwa ajili ya haki za ardhi. Ibara ya 26 inaeleza kuwa:

*“Jamii za wenyeji zina haki ya kumiliki ardhi, maeneo, na rasilimali ambazo wamezimiliki, kuzihodhi, au kuzitumia kienyeji.”*

Kuhusu matumizi ya ardhi, swali kuu linahusu kufasili nafasi ya jamii za wenyeji na dola. Kama ilivyofafanuliwa na Petra, asilimia 90 ya ardhi iliyotumiwa na Wasámi kwa ajili ya ufugaji wa kulungu inasimamiwa na kampuni ya serikali ya Metsähallitus. Hii ina maana kwamba Wasámi na serikali kila upande unadai kuwa na haki ya kumiliki ardhi, jambo linalopelekea kuzuka kwa maslahi kinzani.

Aidha, kuhusu mabadiliko ya tabianchi, Petra alieleza kuwa idadi ya wadau wanaovutiwa na masuala ya eneo la Aktiki imeendelea kuongezeka. Hii ina maana kuwa majadiliano zaidi na zaidi yanaendelea kuhusu mipango tofauti ya matumizi ya ardhi kati ya wadau tofauti na serikali. Kwa mujibu wa sheria ya Kifini ni sharti kuijumuisha jamaii ya Wasámi kwenye majadiliano haya.

Suala la majadiliano haya lilitufikisha kwenye mahitimisho ya Petra. Kwa kuwa kihistoria kumekuwa na hali ya kutoaminiana kati ya serikali na jamii ya Wasámi, kuna wasiwasi kwamba jamii ya Wasámi hawashirikishwi kwa usawa kwenye majadiliano haya. Kukosekana kwa hali ya kuaminiana kumewafanya Wasámi wawe waangalifu sana kuhusu ardhi yao na, kama alivyosema Petra:

■ *"Hawataacha kuipigania."*

Kutokana na kuongezeka kwa maslahi tofauti katika eneo la Aktiki, hali hii inapaswa kubadilishwa ili kulinda ustawi wa Wasámi. Petra alihitimisha wasilisho lake kwa swali linalosisimua:

■ *"Njia ipi inafaa kuzishirikisha pande ambazo haziko tayari kushiriki katika majadiliano?"*

## **Sanaa kama kichocheo cha ufumbuzi wa amani nchini Kolombia**

Wasilisho lililofuata lilitolewa na **Leonardo Párraga**, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la BogotArt na mwanzilishi-mwenza wa kampeni ya Barua za Maridhiano wa nchini Kolombia.

Shirika la BogotArt linajihusisha na matumizi ya sanaa kwa ajili ya ujumuishaji wa kijamii na kuleta amani. Leonardo aliwaambia washiriki wa kongamano kuhusu mradi, ambao lengo lake ni kujenga hali ya kuaminiana na mawasiliano kati ya makundi yenye uhasama wa kihistoria nchini Kolombia.

Leonardo alieleza kuwa mradi huu ulitokana na shauku ya shirika kujaribu kutumia sanaa kuyaleta pamoja makundi yaliyohasimiana. Walianza ngazi ya chini kwa kutumia michoro mikubwa ya ukutani. Kuyapa makundi ya kijamii nafasi ya kuchora michoro mikubwa ya ukutani kwenye majiji kulibainika kuwa njia nzuri ya kuwapa fursa makundi ya kijamii kuelezea utambulisho wao na kuwasiliana na wengine. Kwa kutumia uzoefu huu wa kutia michoro mikubwa jijini Bogotá, Leonardo na wenzake walianza kufikiria wanavyoweza kusambaza wazo hili nchi nzima.

Leonardo alieleza kwamba makubaliano ya amani yaliyosainiwa nchini Kolombia yalisababisha mgogoro na yaliigawa nchi kati ya "sisi" na "wao". Kulikuwa na watu wengi waliopendelea kuwa





na makubaliano ya amani lakini walikuwepo pia waliopinga. Moja ya makundi yaliyokuwa na nguvu ni wapiganaji wa zamani, ambao walizoea kuiona serikali adui yao na isiyoaminika. Kulikuwa na mashauriano hafifu kama si hayakuwepo kabisa kati ya makundi haya jambo lililosababisha uhasama nchini Kolombia.

Kisha, wazo la kuandika barua liliibuka walipofikiria njia za kuwasiliana. Ingawa barua zimegeuka sanaa iliyotoweka, bado zina nguvu na siku za nyuma zimethibitisha kuwa zana madhubuti za kuanzishia mijadala. Leonardo na timu yake walibaini kuwa barua ni fursa ya kuelekeza mijadala katika mwelekeo chanya. Waliwapa watu fursa ya kuandikiana barua, ambapo washiriki walijieleza kwa maneno yao wao ni nani; jinsi walivyoathiriwa na mgogoro; na dira yao katika kuleta amani. Jaribio lao lilifanikiwa sana na zaidi ya watu 3000 walishiriki, hivyo kuwa kampeni ya kitaifa.

Leonardo alisimulia visa vya watu wawili walioshiriki katika kampeni. Kisa cha kwanza kilihusu mpiganaji wa zamani, ambaye kwake

kupokea barua kulibadili maisha yake. Kwa kupokea barua, mpiganaji huyu wa zamani alijisikia amesikilizwa na kupewa msaada. Kwa maraya kwanza maishani mwake alijisikia sehemu ya jamii na aliyethaminiwa kama binadamu. Katika barua yake ya majibu, mpiganaji huyu wa zamani aliandika kwamba hadi wakati huo alikuwa anaona silaha na vurugu ndio njia pekee; lakini hatimaye sasa alikuwa tayari kujifunza stadi mpya za maisha na kuwa sehemu ya jamii ya kiraia.

Katika kisa cha pili, Leonardo alitusimulia kuhusu mtu ambaye familia yake iliua na kikundi cha waasi cha FARC. Maisha yake yote aliishi akitaka kulipiza kisasi na alikuwa akiamini kuwa vurugu ndiyo njia ya kutimiza azma yake. Hata hivyo, kwa kukutana na mpiganaji wa zamani kupitia barua, alitambua kuwa alipaswa kuacha chuki yake na kutafuta njia ya kusamehe ili kujenga jamii bora.

Baada ya visa hivi vya kulisimua, Leonardo alieleza jinsi visa na mgogoro ulioelezwa ulivyohusishwa na ulinzi wa mazingira. Maeneo ambayo yalizoeleka kuwa chini ya kikundi cha



Antti Erkkilä, 2018

waasi cha FARC yalikuwa pia na hifadhi nyingi za asili. Chini ya kikundi cha waasi cha FARC, maeneo haya yalikuwa yanahifadhiwa kwa kiasi fulani kwa kuwa yalikuwa yakitumika kwa kiasi kidogo. Baada ya mkataba wa amani kusainiwa, makampuni na wadau wengine walianza kuhamia kwenye maeneo haya na kulikuwa na hofu kwamba ardhi haitahifadhiwa. Leonardo alihitimisha kwamba wakati ardhi ilikuwa na fursa kubwa ya kuleta utangamano kwa jamii za Kikolombia, kulikuwa na haja ya kutafuta namna ya kusimamia ardhi ili kuzuia kuibuka kwa mgogoro mpya.

### **Mafunzo Yatokanayo na Kozi za Kinodi kuhusu Ushirikiano wa Kimazingira na Usuluhishi wa Migogoro**

Wasilisho la mwisho kwa awamu ya asubuhi lilitolewa na **Emma Luoma** na **Juha Kotilainen**, ambao ni wanafunzi wa PhD katika Chuo Kikuu cha Ufini Mashariki.

Emma na Juha walituletea mafunzo muhimu kadhaa waliyojifunza katika kozi za shule ya majira ya kiangazi ya Kinodi kuhusu ushirikiano wa kimazingira na usuluhishi wa migogoro (soma zaidi [HAPA](#) kuhusu kozi na masomo yake).

Juha alianza kwa kujadili jinsi ambavyo kuna changamoto za kijamii zinazohitaji kushughulikiwa kuhusu matatizo ya kimazingira. Ni nadra sana mgogoro ukahusu maliasili pakee. Kuna uwezekano wa kuwepo masuala yanayohusiana na maadili, madaraka, na miundo ya kijamii, ambayo inaweza kuwa migumu kuitatua. Migogoro ya kimazingira inaweza kujumuisha masuala kutoka maeneo haya yote, na hivyo kuifanya iwe changamano mno.

Aidha, si wakati wote migogoro ni jambo baya; wakati mwingine inaweza kuleta matumaini dhidi ya ukosefu wa haki, na inaweza kutoa fursa ya mabadiliko yanayoweza kuleta hali nzuri. Migogoro ina dhima muhimu, lakini kipaumbee kiwe kuzuia vurugu.

Emma aliendelea kwa kujadili mkabala wa majadiliano unaozingatia maslahi unaojulikana kama mkabala wa manufaa kwa pande zote ambao wamekuwa wakijifunza pamoja na Juha wakati wa kozi. Mkabala huu unajengwa kwa kuzingatia dhana kuwa inawezekana kutafuta

masuluhisho yanayozinufaisha pande zote na hivyo kukubalika zaidi kwa njia ya ushirikiano na majadiliano yanayolenga kufanikisha maslahi ya pande zote. Ushirikiano wa aina hii hauna walioshinda na walioshindwa, bali ushindi unakuwa kwa wote kupitia juhudi za pamoja.

Kama funzo kuu, Emma aliibua umuhimu wa kusikiliza. Ili makundi yanayoshirikiana yapate masuluhisho yanayozinufaisha pande zote, pande hizo zinapaswa kufahamu maslahi yake na maslahi ya pande zingine zinazohusika katika mgogoro. Jambo hili linawezekana kwa njia ya kusikilizana kwa makini. Kama mfano, Emma alielezea hali ambayo mtu ana mihemko na hivyo awezi kushiriki katika majadiliano chanya. Ili kumsaidia aweze kuwa msikivu tena, mtu huyu anapaswa kusikilizwa kwanza.

Somo lingine kutoka kwenye kozi ambalo Juha alilibainisha lilikuwa haja ya kuwa na mtazamo wa kiuhalisia dhidi ya migogoro. Katika hali tete, lengo la mchakato wa usuluhishi haupaswi kuwa makubaliano kamilifu. Wakati mwingine inaweza kuwa uhalisia zaidi na toshelevu kuelekeza mchakato katika moja ya masuala yafuatayo: kiini, taratibu, au mahusiano. Hatua hii pekee inaweza kuwa ushindi mkubwa.

Mwisho, Juha alieleza kuwa inaelekea ni wazi kwamba uzuri wa njia za ushirikiano utaendelea kukua siku zijazo. Matatizo tatanishi, yenye changamoto zaidi, na ya kimazingira ya dunia yanayoongezeka yakichanganywa na dhima inayobadilika ya dola na jumuiya za kiraia, yataongeza msukumo wa mikabala jumuishi na ya ushirikiano. Juha na Emma walihitimisha kwa kusesitiza kuwa tunawahitaji vijana wenye shauku ya kufanya aina hii ya kazi wakati huu – kuliko ilivyokuwa hapo awali.

### **Mjadala**

Baada ya mawasilisho, ukumbi ulikuwa wazi kwa ajili ya maoni na maswali yoyote. Kulikuwa na maswali mahususi kuhusu masuala yaliyowasilishwa, pamoja na tafakuri na hisia pana zaidi zilizotolewa na washiriki. Dhima ya uanaharakati na vuguvugu la mabadiliko ya tabianchi ilijadiliwa kwa mitazamo tofauti tofauti, na tofauti baina ya nchi zilizowakilishwa zilizingatiwa pia.

Jambo la kwanza lililoibuka katika mjadala lilikuwa muundo changamani na anuai wa migogoro mingi. Kuna aina nyingi za changamoto za kijamii, kama tulivyosikia katika mawasilisho ya awamu ya asubuhi. Kuandamana katika nchi ambayo unakaribishwa na risasi si chaguo. Hivyo, unapaswa kuwa mbunifu na kuonesha njia, mathalani kwa kukusanya taka. Rushwa na kuihusisha kwa makusudi migogoro na siasa pamoja na migawanyiko ya kifikra ni masuala yanayopaswa kushughulikiwa.

Kimsingi, mabadiliko ya tabianchi ni mfano wa masuala yanayohitaji kutatua matatizo kadhaa kwa wakati mmoja ili kupata masuluhisho endelevu. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, nchi zinakabiliwa na aina tofauti za vitisho vya migogoro vinavyotegemea si tu hali za kiuchumi, kiikolojia, na kijamii bali kwa historia yake. Yote haya yanapaswa kuzingatiwa wakati wa kujadili masuluhisho ya migogoro.

Jambo la pili lililoibuliwa katika mjadala lilikuwa hisia kuwa hatuko peke yetu katika matatizo yetu. Kuna watu wengi duniani wanaojitahidi na kujaribu kutatua masuala haya. Tunahusiana zaidi kuliko tunavyodhani. Watu walihisi kuna fursa kubwa katika mahusiano na uwezo wa pamoja unaojengwa ulimwenguni kote.

Jambo la tatu, ambalo linahusiana sana na la pili lilikuwa wito wa uwepo wa uhamasishaji. Ni

kwa namna gani tutaondokana na ushirikiano huu tengani na badala yake kuelekea katika vuguvugu jumuishi zaidi zinazoweza kuvuka mipaka ya migawanyiko? Kulitolewa wito wa kuwa na aina mpya ya mapinduzi: mapinduzi yanayojengwa katika misingi ya mshikamano badala ya vurugu.

Ilibainika pia kuwa ni muhimu kujaribu na kuzuia vuguvugu za tabianchi kuwa ni vuguvugu za tabaka la wasomi pekee. Kama ilivyoielezwa katika mawasilisho, tayari inaweza kuonekana kuwa vuguvugu zinazohusu mabadiliko ya tabianchi zinakua kwa kasi katika nchi ambazo zimeathiriwa kwa kiasi kidogo na mabadiliko ya tabianchi, ambapo ni hatari zaidi kuwa sehemu ya vuguvugu za kisiasa katika nchi ambazo tayari zinaathiriwa na athari kubwa za ongezeko la joto na ambako migogoro inaendelea. Ingawa vijana wakiungana wanaweza kutekeleza dhima muhimu katika masuluhisho, hawawezi kuachiwa jukumu lote; watu wazima, wafanya maamuzi na wasomi wanapaswa pia kutimiza wajibu wao wakati wakizingatia rasilimali zilizopo.

### 3. Mjadala wa Kikundi Kidogo cha World Café

Awamu ya mchana ilianza na mjadala wa kikundi cha World Café kuhusu maswali matatu tofauti yaliyohusiana na ushirikiano wa kimazingira



na michakato ya amani. Kwa ujumla, njia hii ilijumuisha duru kadhaa, ambapo washiriki walibadilishana meza na mada, na kuendeleza mjadala uliofanyika katika duru zilizotangulia katika meza husika. Kulikuwa na vikundi vitatu na meza tatu za mada au maswali elekezi. Duru tatu za dakika 20 zilitoa fursa ya kutosha ya mjadala kuhusu mada husika. Muhtasari ufuatao unazingatia masuala yaliyoibuliwa na waratibu wa meza **Daniela Tináková, Violeta Gutiérrez** na **Denis Dobrynin**.

***Wewe au vijana kwa ujumla wanakabiliana na aina gani ya migogoro ya kimazingira nchini mwako?***

Washiriki walitoa mifano tofautitofauti ya migogoro, kuanzia ngazi ya familia hadi taifa na hata migogoro ya kiulimwengu, ambamo vijana wana wajibu wa kutekeleza. Mifano hii ilihusiana na masuala ya maji, uharibifu wa misitu, kilimo, uvuvi uliopitiliza kiwango, uchafuzi wa mazingira, uzalishaji wa nishati, ujenzi wa miundombinu, udhibiti wa taka, na migogoro kati ya binadamu na wanyama. Vijana walishirikishwa kupitia asasi zisizo za serikali na maeneo ya wakazi asilia.

Ilibainika kwamba kuna tofauti za kivitazi.

Vizazi chipukizi vina mtazamo tofauti kuhusu, mathalani, misitu. Mitazamo hii si lazima ihusiane na fedha na inaweza kukinzana na mingine. Ilikezwa kwamba vijana wanaweza kuwa na mtazamo chanya dhidi ya mazingira na malengo tofauti ya maisha kuliko kizazi cha watu wazima. Mabadiliko ya tabianchi yanaweza kuangaliwa pia kama mgogoro kati ya vizazi. Hata hivyo, ni muhimu kujumuisha vikundi vya wadau wa rika tofauti katika mchakato wowote wa ushirikiano kwa sababu wanaleta mitazamo tofauti tofauti.

Kila kikundi kiligusia pia suala la taarifa na athari zinazohusiana na, mathalani, taarifa kinzani na habari za uongo. Ilionekana kuwa ni muhimu watu wafundishwe shuleni kufikiri kwa kina ili waweze kuchakata aina mbalimbali za taarifa kutoka vyanzo tofauti, ambavyo vinaweza kuwa na ajenda tofauti. Ni muhimu kueneza sayansi lakini siyo kuirahisisha mno. Vijana huwasiliana kwa namna tofauti kuliko watu wazima, mfano kwa kutumia mitandao ya kijamii.

***Ni aina gani ya ushirikiano wa kimazingira na mbinu au mienendo ya usuluhishi inayotumiwa na inayoweza kutumiwa na vijana?***



Mada muhimu iliyojadiliwa ilikuwa umuhimu wa dhima ya stadi za uwezeshaji na usuluhishi katika ujenzi wa ushirikiano wa kimazingira, kusaidia kujenga hali ya kuaminiana, na kuwapa fursa ya kupaza sauti wadau mbalimbali wanaohusika katika migogoro na ufanyaji maamuzi. Kwa watafiti chipukizi, inafaa kujifunza stadi hizi zinazotoa zana za kushughulikia masuala mbalimbali ya kazi zao na hata kwa maisha yao ya kawaida. Aidha, hizi ni stadi zinazoweza kufundishwa shuleni katika hatua za awali za elimu ili watoto wajifunze kutatua migogoro na kuleta amani.

Mitandao ya kijamii inaweza kuwa na dhima muhimu kwa vijana katika kutafuta watu wenye fikra zinazoendana, kuwaleta pamoja watu hawa, na kuwa hai katika kuelezea mawazo yao. Mitandao ya kijamii inaweza kuwapa vijana zana nyingi zaidi za ushawishi. Ilibainika kuwa wakati mitandao ya kijamii inaweza kuwa zana ya kufanyia mijadala, haiwezi kuwa peke yake; kuna suala la ujumuishi pia.

Mitandao ya kijamii ilionekana pia kuwa zana madhubuti kwa ajili ya uhamasishaji. Mshiriki mmoja alibainisha kuwa inaweza pia kusababisha changamoto kwa usuluhishi wa ndani wa migogoro kwa sababu huleta migogoro kwenye “mjadala wa wazi” na wenyeji hawana muda wa kutosha kushughulikia migogoro wao peke yao. Uhakikifu wa mitandao ya kijamii ulihojiwa pia na dhima yake katika kuleta mgawanyiko wa mitazamo ya jamii.

Umuhimu wa mitandao uliibuliwa pia. Mshiriki mmoja alisema kwamba:

*“Si lazima uwe usuluhishi wa moja kwa moja, bali mtandao wa watu wenye fikra za aina moja zinazoleta mabadiliko ya mielekeo ya mgogoro, na watu huona fursa za kila mmoja; kwa sababu, unapobaki kwenye muktadha wako, huwezi kuona mlango wa kutokea.”*

Kwa mujibu wa mshiriki mmoja, katika mchakato wa kuleta amani, kudhani na uwezekano wa uwepo wa masuluhisho tofautitofauti ni muhimu, na mitandao na vuguvugu zina dhima muhimu.

Washiriki waliibua stadi na hali kadhaa muhimu, ambazo zinaweza kutumika kuanzisha ushirikiano wa kimazingira na kushughulikia

mifumo ya mchakato wowote:

- Kusikiliza kwa makini
- Kujenga hali ya kuaminiana
- Uwazi
- Ufuatiliaji wa pamoja wa utekelezaji
- Maarifa kuhusu muktadha
- Uhakika wa usalama kwa wahusika
- Muda na fedha

### ***Ni vihatarishi gani vinavyohusisha vijana katika ushirikiano wa kimazingira na usuluhishi wa migogoro?***

Katika mjadala, vihatarishi viligawanywa katika makundi mawili. Kwanza, vihatarishi kwa vijana wenyewe. Ushiriki katika shughuli za kimazingira unaweza kuwa na athari hasi kwa afya ya vijana, kwa kuwa shughuli zinaweza kusababisha msongo wa mawazo na kusababisha, kwa mfano, kukosa usingizi. Katika mazingira ambayo hakuna mabadiliko ya haraka na matokeo ya maana yanayopatikana, huweza kusababisha vijana kuchanganyikiwa na hivyo, katika baadhi ya mazingira, kusababisha watu kutoshiriki tena. Ushiriki unaweza pia kusababisha uchovu iwapo vijana wamedhamiria haswa kujitua na shughuli yenyewe kuwa kipaumbele katika maisha yao. Uanaharakati wa mazingira huweza kutumia muda mwingi, na hivyo kuendelea na maisha ya kawaida (shule, kazi, n.k.) na kudumisha mahusiano ya kifamilia inaweza kuwa vigumu.

Suala lingine lililoibuliwa lilihusu hatari ya unyanyapaa wa wanaharakati vijana. Kwa upande mmoja inaweza kuwa suala hasi na mzigo mzito. Kwa upande mwingine, uzoefu katika uanaharakati huweza kuonekana wa thamani.

Mtazamo wa kulisimua ulikuwa kwamba tunaweza tukawa tunawapa vijana msukumo mkubwa, na kunaweza kuwa na athari hasi iwapo hawashiriki siasa. Vijana hawapaswi kulazimishwa kuingia kwenye uanaharakati na wanatakiwa waweze kuamua cha kufanya kwa kuzingatia uwezo na matakwa yao.

Vihatarishi vikubwa zaidi kwa vijana vilivyobainishwa katika ushirikiano wa kimazingira na usuluhishi wa migogoro ni kudhurika moja kwa moja na ukosefu wa usalama unaoweza kutokea katika baadhi ya mazingira. Vihatarishi

hivi vinaweza kutofautiana kwa kiasi kikubwa kati ya maeneo tofauti ulimwenguni. Katika baadhi ya nchi na tamaduni, kujihusisha na uanaharakati kunaweza kusababisha kutengwa na jamii na familia, kwa kuwa, mathalani, mtu lazima aheshimu mawazo ya familia.

Kundi la pili la vihatarishi kwa vijana lilihusu michakato ya ushirikiano na kuleta amani. Hali ya kuchanganyikiwa na ukosefu wa matokeo ya haraka ulioelezwa awali unaweza kusababisha misimamo mikali na vurugu. Hata kama mabadiliko chanya yanatokea, kasi ya utokeaji inaweza kuonekana ni ya taratibu sana.

Dhima ya uanaharakati katika michakato ya migogoro ilijadiliwapia. Mshiriki mmoja alibainisha kuwa njia ya uanaharakati inapaswa isailiwe na kwamba wakati mwingine uanaharakati wa ushawishi unaweza kufanya mambo yakawa mabaya zaidi na kuchochea migogoro. Aina hii ya uanaharakati haitafuti ufumbuzi au kushirikiana, na pengine haifai. Mshiriki mwingine alipinga mtazamo huu na aliona kwamba wakati mwingine unahitaji aina hii ya uanaharakati ili kutengeneza fursa ya kuwa na uanaharakati unaozingatia ushirikiano wa kihuduma zaidi.

## 4. Mjadala wa jopo

Mjadala wa jopo ulioongozwa na **Irmeli Mustalahti**, ulijumuisha mihtasari ya waratibu wa meza na maswali yaliyobuniwa kuhusisha mada na masuala mengine pia.

Katika sehemu ya mwanzo ya awamu hii, kulikuwa na mjadala uliogusia vyanzo vya migogoro. Dhana ya migogoro ya kimazingira ilisailiwa kwa sababu kwa kawaida kuna masuala kadhaa wanayoathiri sambamba na kuzuka kwa migogoro. Ilielezwa kuwa ni sahihi zaidi kusema migogoro mingi ina chembechembe za kimazingira. Migogoro ni sehemu ya maisha na inaweza kuwa vyanzo vya mabadiliko. Mshiriki mwingine aliunga mkono mtazamo huu na aliona migogoro au majanga ni vichocheo vya mabadiliko. Huashiria kuwa jambo fulani halikushughulikiwa. Hivyo, sasa tunaweza kuwaza: tufanye nini, tufanyeje ili kubadili hali iliyopo ili iwe bora?

Swali hili lilipelekea mjadala wa mabadiliko ya namna watu wanavyokabili mchakato wa kuleta amani. Mwanzoni ilikuwa kuhusu **usuluhishi wa migogoro**: jinsi gani ya kusuluhisha migogoro?

Swali hili lilifuatiwa na **udhibiti wa migogoro**: tunadhibitije baada ya kupatikana kwa suluhu ya migogoro? Sasa tunazungumza kuhusu **mageuzi ya migogoro**: migogoro inaonekana ni fursa ya kufikiria uwezekano tofauti, kama fursa ya kuleta mageuzi. Sasa hivi si usuluhishi unaofanyika vyumbani; mageuzi sasa yanachukuliwa kuwa ni yale yanayotokea katika masuala mtambuka, katika jamii mbalimbali, katika vizazi tofautitofauti.

Mada nyingine katika mjadala ilikuwa vihatarishi vya uanaharakati wa vijana. Mmoja wa washiriki alieleza kuwa katika baadhi ya nchi, kuwa mwanaharakati kunaweza kuathiri masuala ya kazi ya mtu kama uanaharakati haukubaliki. Ilielezwa pia kuwa uanaharakati unaweza kuwa kazi ngumu na wakati mwingine hutumia muda mwingi. Hata hivyo, uanaharakati ulionekana ni njia muhimu ya kuwa mwanajamii hai na nyenzo ya kutekelezea masuala ambayo vijana wanayaamini.

Katika muktadha huu, hoja ilitolewa kuhusu suala la vihatarishi kwa vijana wanaojihusisha na ushirikiano na mazingira ya migogoro (tazama mjadala wa World Café hapo juu). Labda ingefaa kujielekeza katika changamoto za kuwashirikisha vijana na jinsi ya kutatua masuala haya badala ya kuorodhesha mambo ambayo ni magumu au ambayo yanaweza kuwazuia vijana kushiriki. Unaweza kuona jinsi aina hii ya orodha inavyoweza kumkatisha mtu tamaa ya kushiriki katika harakati na kupigania masuala muhimu yanayofaa kujitolea mhanga. Ilielezwa kuwa, kwa vijana hawa, kujaribu kutafuta aina fulani ya mtandao saidizi kunaweza kusaidia, hata kama hawapati msaada kutoka kwenye familia zao.

Tukirejea kwenye sababu za migogoro, ilielezwa kuwa migogoro kwa kawaida huhusu ukosefu wa mawasiliano na maelewano. Kama kutafunguliwa njia mpya za mawasiliano, tunaweza kuimarisha maelewano na kusonga hatua moja mbele. Moja ya misingi ya usuluhishi wa amani ni kwamba unapaswa kufahamu maslahi ya pande zote zinazohusika ili uweze kupata suluhu. Kwa njia hii, migogoro inaweza kuzisaidia jamii kuanzisha majadiliano kuhusu sababu za migogoro na hivyo kusaidia kujenga hali ya kuaminiana baina ya pande zinazohasimiana.

Hoja kama hizi zilitolewa wakati wa kusisitiza umuhimu wa kazi za maandalizi ya usuluhishi

au ushirikiano wa kimazingira. Kuna vikundi na taasisi tofauti zenye maslahi ambazo zinahusika haswa na matatizo yaliyopo ambazo ni nadra kuonekana au uhusiano huo hauonekani. Ni muhimu kuwahusisha wote. Kwa mfano, katika migogoro inayohusiana na misitu, unaweza kusema kuwa wamiliki wa ardhi na serikali wanaonekana bayana na ni sehemu muhimu ya mgogoro. Hata hivyo, wanaharakati na watoto wa chekechea katika maeneo husika wanaotumia misitu ni muhimu pia – wanaweza kuwa na mchango muhimu katika suluhu. Hivyo, unapaswa kutekeleza wajibu wako vizuri sana na kufikiria nani washiriki katika mazungumzo wakati maswali haya yatakapoulizwa. Ni ngumu na huhitaji muda mwingi lakini hivi ndivyo unavyopaswa kufanya na kuwa navyo.

Mshiriki mmoja katika mjadala wa jopo alieleza kuwa ni mabadiliko makubwa hasa kwamba tofauti na miaka ya 1980 na 1990, sasa vijana hawaogopi unyanyapaa wa uanaharakati. Hata hivyo, katika baadhi ya nchi, unyanyapaa haukomi baada ya miaka kadhaa bali huweza kudumu maisha yote. Aliendelea na swali la tafakuri binafsi: je, tunawatupa vijana katikati ya supu, ambayo ni migogoro bila ya kuwapa usaidizi unaohitajika? Tunapaswa kuwa makini ili tusiwatupe vijana humo bila kuelewa jinsi ya kuwalinda na gharama watakazolingia. Ndiyo maana tupo hapa leo pia: kuelewa aina ya supu ambayo tunawatupa vijana hawa.

Hoja hii ilitolewa na mshiriki mwingine aliyehoji mtazamo kwamba vijana wanaonekana kuwa waathirika wanaotupwa mahali fulani au kama vitu tu visivyojimudu vinavyotumika katika miktadha ambayo tayari ipo. Vijana tayari wamo ndani ya supu na wanatambua sana kinachotengeneza ladha ya supu. Hivyo, pengine badala ya kufikiria kuhusu iwapo supu ina joto sana au jinsi ya kuwaopoa vijana kutoka humo, itafaa zaidi na itaendana pia na michakato ya Umoja wa Mataifa, kufikiria kuhusu: kwa nini tayari vijana wamo humo; na supu inaundwa na nini?

## 5. Hitimisho

Migogoro mikubwa ya kimazingira ulimwenguni kote mara nyingi inahusiana na matumizi ya mailiasili za kikanda na za kienyeji, kama vile rasilimali za mafuta nchini Najeria, madini nchi za Latini Amerika, au upatikanaji wa maji safi

ulimwenguni kote. Ingawa changamoto zinaweza kuwa za kikanda na migogoro kuwa ya kienyeji, njia za makusudi na shirikishi za kuchambua miktadha na hali za migogoro inaweza kutumika katika mazingira mbalimbali ya migogoro. Kusikiliza kwa makini maslahi, mahitaji, na mitazamo ya kila mmoja bila kuhukumiana ni muhimu sana na ni stadi ya msingi ya uchambuzi wa migogoro na mbinu za usuluhishi.

Katika Tukio hili la Kando, mkazo wetu ulikuwa misugvano na migogoro inayoweza kusuluhishwa kwa njia ya hatua laini za kiusalama katika maeneo ya wenyeji. Masuala ya msingi ya migogoro ya kisiasa yanaweza kujumuisha masuala kama vile migogoro ya matumizi ya ardhi na migogoro ya matumizi ya maliasili. Migogoro inayohusiana na maliasili (maji, misitu, uhifadhi, matumizi ya ardhi, madini, n.k.) inaweza kuwa mwanzo wa michakato ya kitaifa ya kuleta amani. Na vijana wanaweza kuwa watu muhimu wa kuenezastadi za msingi za ushirikiano wa kimazingira na usuluhishi wa migogoro ya kimazingira. Kufundisha stadi hizi kunapaswa kuonwa kama elimu ya uraia, kama ilivyo kwa stadi za huduma ya kwanza.

Kuna masuala matatu ya kipaumbele ambayo vijana wanaweza kushirikishwa na kufundishwa zaidi kupitia stadi zinazozingatia utendaji:

**Kubuni** hatua na zana laini za kiusalama kupitia mienendo ya kiushirikiano na inayohusisha wadau mbalimbali.

**Kusaidia** na kubuni stadi za kuunda matendo shirikishi.

**Kujifunza** zana/stadi za kusikiliza kwa makini kivitendo katika kupima na kusuluhisha mazingira ya migogoro.

Hatua na zana laini za kiusalama husaidia ujenzi mpya wa jamii na kuwezesha ushirikiano baina ya wadau mbalimbali, ikiwa pamoja na mchango ya vijana. Uwezeshaji wa mjadala na sekta zenye mahitaji ya ajira, kunaweza kutoa hatua laini za kiusalama ambapo vijana wanaweza kushiriki shughuli za kiushirikiano na sekta mchanganyiko. Ukuzaji wa stadi za kazi za marika tofauti unaweza kuwa aina mojawapo ya zana laini za usalama ili kusaidia ujenzi wa jamii mpya.

Umuhimu wa usikilizaji makini hauwezi kupuuzwa. Hali za migogoro huchosha na hisia za kutosikilizwa mara nyingi hutokana na kukosekana kwa hali ya kuaminiana na kunaweza kusababisha kuzuka kwa vurugu. Katika migogoro ya kimazingira, mara nyingi watu hushindwa kusikiliza jambo lolote, liwe la maana au la, hususani wanapokuwa wamechanganyikiwa na wenye hasira. Hali hii huzuia uwezo wa kuchakata taarifa zozote mpya, hususani kwa vijana na watu wasio na uzoefu wa awali unaoweza kuwasaidia kutafakari na kusuluhisha migogoro.

Tunapaswa kuwa waangalifu ili “vijana wasibebeshwe jukumu” la kurejesha imani katika kipindi cha baada ya migogoro au vita, wakati ambapo mantiki ya uwajibishaji iliyo katika juhudi za serikali ya kileo inashindwa na badala yake migogoro hushika hatamu. Uanuai wa mipango ya kiutawala katika kipindi cha baada ya vita au mazingira ya baada ya migogoro unahusishwa na utegemezi wa kuwabebecha watu wajibu wa ustawi wao (pia kwa matokeo yanayohusiana na rasilimali).

Mikakati ya kuwafanya watu wawajibike kwa ustawi wao ni sifa inayoendana na mapinduzi yanayoendelea ya utawala katika ngazi zingine za kijamii, kama vile magonjwa na afya, elimu, uhalifu na sheria, na usimamizi wa gharama za biashara. Kwa ujumla, ushiriki na ujumuishaji wa vijana kwa ajili ya kuzuia na kusuluhisha migogoro unahitaji pia juhudi za muda mrefu za dola ili kuhakikisha kuna ulinzi wa kijamii wa wapigakura vijana.

Juhudi za usuluhishi zinazoongozwa na vijana zinahitaji ujumuishaji wa kanuni muhimu na “zisizodhuru”. Juhudi za usuluhishi pamoja na michakato ya ushirikiano ni michakato ya muda mrefu ya mageuzi inayohitaji muda, utambuzi wa mizizi ya migogoro, na mashauriano ili kiheshima kutengeneza upya mfumo wa “matukio” na “kweli” zilizoanzisha na kuchochea migogoro. Vijana wanaoshirikishwa katika aina hizi za michakato hii mirefu wanahitaji ulinzi wa haki zao, ikiwa ni pamoja na haki ya kujitoa kwenye michakato hii pale nafasi zao za kijamii au maisha yao binafsi na familia zinapokuwa hatarini.

## Shukrani

Tukio la Kando liliandaliwa na miradi ya ALL-YOUTH na CORE iliyofadhiliwa na Baraza la Utafiti wa Kimkakati (SRC) [ruzuku na. 312689 na 313013], Mradi wa MAKUTANO uliofadhiliwa na Akademia ya Ufini [ruzuku na. 320236] na ALLIANSSI, Shirika la Vijana la Ufini. Ukumbi wa Tukio la Kando, Think Corner, ulitolewa na Chuo Kikuu cha Helsinki. Tunashukuru pia kwa msaada wa kifedha wa nyongeza kutoka Chuo Kikuu cha Ufini Mashariki pamoja na ushirikiano muhimu wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufini, hususani Outi Hakanen, Laura Kaltiainen, na Eero Väisänen. Tunamshukuru pia Rajabu A. Chipila wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kutafsiri ripoti hii kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili.

---



## Waandaaji

**MAKUTANO Mradi wa kujenga ushirikiano na utatuzi wa migogoro ya misitu** ni mradi unaofadhiliwa na Programu ya Akademia ya Maendeleo (2019-2022), ambayo ni programu iliyoandaliwa kwa pamoja kati ya Akademia ya Ufini na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufini. Lengo kuu la mradi huu ni kuchunguza stadi za ushirikiano wa kimazingira na njia za usuluhishi wa migogoro miongoni mwa wamiliki wa misitu na wanajamii katika Nyanda za Juu Kusini nchini Tanzania; na kuangalia jinsi stadi hizi zinavyobadilishwa na kutumiwa katika hatua za siku zijazo zinazochukuliwa na wamiliki hawa na jamii zinazoizunguka misitu hiyo. Ushirikiano huu wa kitafiti unajumuisha washirika wa kimataifa kutoka Tanzania, Kenya, Meksiko, na Denmaki.

**ALL-YOUTH linataka kutawala ulimwengu wao** ni mradi wa taaluma mchanganyiko (2018-2023) unaochunguza uwezo wa vijana (wenye umri wa kuanzia miaka 16 hadi 25) na vikwazo vinavyowakwamisha kushirikiana na jamii zao. Shabaha kuu ya mradi huu ni kutengeneza uwezekano na kuwawezesha vijana kushiriki katika kuunda jumuiya na jamii zao. Mkazo wa utafiti huu umewekwa katika utawala wa kiuwajibikaji na utawala wa sheria, ugunduzi wa kidigitali, na juhudi za maendeleo endelevu, kama vile uchumi-biolojia wa misitu. Mradi wa ALL-YOUTH unafadhiliwa na Baraza la Utafiti wa Kimkakati (SRC) chini ya Akademia ya Ufini.

**CORE Uponyaji wa pamoja wa jamii zilizofarakana** ni mradi wa utafiti (2017-2021) unaotokana na dhana za utawala wa kutegemeana na kushirikiana kama nyenzo za kushughulikia matatizo ya kijamii. Mradi huu unachunguza mienendo inayobuni ufumbuzi wa haki, madhubuti, na unaozingatia maarifa kwa matatizo changamani yanayohusu mazingira na matumizi ya maliasili. Shabaha ya mradi huu ni kutengeneza mbinu za utatuzi wa pamoja wa matatizo katika muktadha wa Kifini na katika kusaidia uwezo wa wadau mbalimbali ili waweze kuzitumia. Mradi wa CORE unafadhiliwa na Baraza la Utafiti wa Kimkakati (SRC) chini ya Akademia ya Ufini.

**ALLIANSSI, Shirika la Vijana wa Kifini** ni taasisi ya huduma kwa taifa na taasisi ya maslahi chini ya kitengo cha kazi kwa vijana. Ni shirika lisilofungamana na itikadi za kisiasa au kidini, ambalo linasimamia asasi za kitaifa 125 za kazi kwa vijana na elimu. Madhumuni yake ni kukuza maendeleo ya vijana ili wawe wanajamii wawajibikaji na kuhimiza ushiriki wa vijana katika ufanyaji maamuzi na shughuli za kimataifa.



*"No one is born a good citizen; no nation is born a democracy. Rather, both are processes that continue to evolve over a lifetime. Young people must be included from birth. A society that cuts off from its youth severs its lifeline." - Kofi Annan, 1998*

## YOUTH PARTICIPATION IN ENVIRONMENTAL COLLABORATION AND PEACE PROCESSES

7 March 2019

**Venue:** Think Corner - Tiedekulma, University of Helsinki, Yliopistonkatu 4, Helsinki, Finland

### PROGRAMME

- 11:00** Opening words, **Reetta Toivanen**, Leader of ALL-YOUTH Research Consortium (STN), Professor of Sustainability Science
- Facilitators: **Heta Heiskanen** and **Antti Erkkilä**
- Realities and lessons learnt around the world and inspirations from the Finnish youth on issues related to environmental collaboration and peace processes
- Finnish youth in action on climate change: **Joel Linnainmäki**
- Climate change realities in Sri Lanka: **Suchith Abeyewickreme**
- Gender and minority aspects of peacekeeping in Lebanon and Kosovo: **Kethlin Piirma**
- Nadafa Le Beledna campaign in South Sudan: **Wani Michael**
- Sámi people and the conflicting land use interests in northern Finland: **Petra Laiti**
- The arts as a catalyzer for peaceful solutions in Colombia: **Leonardo Párraga**
- Lessons learnt from [Nordic courses on Environmental Collaboration and Conflict Resolution](#), **Juha M. Kotilainen** and **Emma Luoma**, University of Eastern Finland
- Discussion
- 13:00** Vegan snack
- 13:30** World Café Small Group Dialogues on environmental collaboration and peace processes
- 15:00** Plenary discussion lead by **Irmeli Mustalahti**, Interaction Coordinator of the ALL-YOUTH Research Consortium (STN), Professor of Natural Resources Governance
- 16:00** Short film

Event Coordinator:

Antti Erkkilä, University of Eastern Finland, [antti.erkkila\[at\]uef.fi](mailto:antti.erkkila[at]uef.fi), Tel. +358 50 595 8381



UNIVERSITY OF  
EASTERN FINLAND

2020

